Yale ambayo vyama vya wafanya kazi vinaweza kufanya

7.1	Usuli	37
7.2	Kuwapanga wakulima wadogo	37
7.3	Kujenga miungano	37
7.4	Jinsi ya kuwapanga wakulima wadogo kwa namna ya kudumu	38
7.5	Tafiti mbalimbali	39
7.6	Ajira ya watoto	40

KUPIMA MAJANI CHAI, KITABU CHA PICHA, PICHA NA.52

7

Yale ambayo vyama vya wafanya kazi vinaweza kufanya

Vyama vya wafanya kazi vina wajibu mkuu wa kutekeleza ili kuinua hali za kikazi miongoni mwa wakulima wadogo, wafanya kazi na wengineo. Hata hivyo, sifa mahsusi za mashamba madogo zinaweza kusababisha changamoto muhimu katika utekelezaji huo. Sehemu hii ya mwongozo inapendekeza baadhi ya mawazo ya kuchukuliwa hatua, na inatoa tafiti mbalimbali za shughuli na kampeni zilizofanikiwa.

7.1 Usuli

Sekta ya kilimo imeajiri asilimia hamsini ya wafanya kazi wote ulimwenguni. Hata hivyo mchanganyiko wa wafanya kazi unabadilika. Asilimia ya vibarua inaongezeka, hususan miongoni mwa wanawake, kwa kuwa wakulima wadogo wanaondolewa mashambani mwao kwa sababu za kisiasa au kwa sababu hawawezi kuendelea kuishi kwa kutegemea mapato ya mazao yao na kwa hivyo wanatafuta ajira kama wafanya kazi wa kilimo. Mashamba makubwa yanawapanga upya na kuwatumia wakulima wadogo kama wakulima wa kandokando/makontrakta.

7.2 Kuwapanga wakulima wadogo

Katika utambuzi wa mabadiliko haya vyama vingi vya wafanya kazi sasa vinatambua haki za wafanya kazi, na wazalishaji wasiokuwa na mishahara kujiunga na vyama hivyo.

Kwa mfano, mnamo mwaka wa 2002, Umoja wa Kimataifa wa Vyama vya Wafanya Kazi wa Maankuli, Kilimo, Hoteli, Mikahawa, Uandazi wa Vyakula, Tumbaku na wengineo (IUF) ulibadilisha sheria zake kwa kufuta marejeo ya vibarua na badala yake kuweka uanishaji mpana zaidi wa 'wafanya kazi'. Hii inajumuisha wazalishaji wadogo na familia zao waliojiajiri, wakulima waliokodi mashamba, makontrakta wadogo na wakulima wasiokuwa na mashamba. Umoja wa IUF umeshirikisha vyama vya wafanya kazi wa kilimo vinavyowakilisha wafanya kazi wasiokuwa na ujira pamoja na mashirika mengi yenye mikakati ambayo pia yamekuwa washiriki. Umoja huu wa IUF unatambua kwamba hakuna mfano au muundo mmoja wa shirika utakaowafaa washiriki wote ijapokuwa kuna kanuni za jumla zinazohimili mifano ya kitaifa.

7.3 Kujenga miungano

Changamoto kwa vyama vya wafanya kazi ni kuwapanga wanaohusika na kilimo, ikiwa ni pamoja na wale wasiokuwa na historia ya muungano wa kidemokrasia. Hata hivyo, vyama vya wafanya kazi vina nafasi nzuri ya kuhamasisha na kuhusisha jamii. Miungano inaweza kujengwa baina ya wafanya kazi wa maankuli, wa mashamba na wazalishaji wadogo ili kuunda mashirika ya kudumu na yaliyo huru. Vyama vya wafanya kazi vinaweza kurekebisha miundo yao ili viweze kushughulikia matatizo ya wazalishaji waliojiajiri na wale wadogo. Vilevile, vyama vya wafanya kazi vinaweza kutoa miundo inayotekelezwa na iliyo na utaratibu wa kidemokrasia katika kiwango cha kitaifa pamoja na kukusanya fedha ambazo zinawasaidia kudumisha uhuru wao.

Miungano pia inahitaji kujengwa na mashirika yanayotoa huduma za jamii na msaada wa uzalishajiwa kiufundi kama vile STEP YA ILO (Strategies and Tools and Social Exclusion and Poverty) na Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) ambalo linatoa huduma za usaidizi kwa wakulima na wafanya kazi wa kilimo. STEP inasaidia upanuzi wa kinga ya jamii katika afya ya wafanya kazi wote, hususan katika sekta isiyo rasmi.

STEP inafanya kazi na jamii vijijini na vyama inavyounga mkono, huduma za usaidizi na inatoa mikopo midogo kwa vyama vya wakulima wadogo. Pia ina mahusiano ya kikazi na mashirika ya Umoja wa Mataifa (Shirika la Afya Ulimwenguni, UNICEF na Mpango wa Maendelo wa Umoja wa Mataifa), Mashirika yasiyo ya kiserkali, vyama vya ushirika na taasisi za utafiti. Mifano ya kazi za STEP ni pamoja na mipango ya afya iliyofaulu ili kuinua hali za kikazi katika kilimo; kusaidia usawa wa kijinsia na kupunguza umaskini wa vijijinil; mipango ya kuzuia ukimwi; kuanzisha uhusiano baina ya kundi lao la mashirika na kupashana habari.

Mamlaka ya Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), kama ajenti wa Umoja wa Mataifa (UN), ni kufanya kazi ili kuzuia ukosefu wa chakula pamoja na kupunguza umasikini. Shughuli zake nyingi zinalenga kutoa usaidizi wa kiufundi na huduma za misaada ya kifedha kwa wakulima wadogo na wafanya kazi wa sekta ya kilimo. Huko Uganda, wakulima wanapata habari kuhusu huduma, teknolojia, soko, mafunzo ya udhibiti wa ubora na mipango ya misaada ya kifedha. Nako huko Msumbiji FAO imeanzisha vilabu vya uwekaji akiba ili kuinua uzalishaji na usalama wa chakula kupitia teknolojia na mifumo ya unyunyiziaji mashamba maji. Hivi majuzi FAO imeanzisha viungo vya moja kwa moja na ofisi za mkoa za IUF pamoja na washiriki wake. Inashirikiana na OXFAM UK, Land Net na Land Net East Africa.

7.4 Jinsi ya kuwapanga wakulima wadogo kwa njia ya kudumu.

Vyama vya wafanya kazi vinahitaji kutambua mahitaji mahsusi ya wakulima wadogo, kwa mfano, uhakika wa kumiliki na kutoa huduma na usaidizi unaofaa. Mahitaji ya wakulima wadogo, kama yalivyoelezwa katika **sura ya 2,** ni kuwa na uwezo wa kufikia mitandao, ambayo matokeo yake ni kuweza kupata maji, vifaa, mbinu za uzalishaji, mikopo, usaidizi wa kisheria na masoko. Mabadiliko ya umiliki ardhi pia ni suala muhimu ikiwa vyama vya wafanya kazi vitapunguza umaskini, ukosefu wa ajira na vurugu. Hii inaweza kuleta udhibiti wa uzalishaji na uuzaji, pamoja na kuhakikisha uzalishaji salama wa chakula, uhifadhi wa mzingara na viumbe hai pamoja na kuhifadhi mbegu asilia. Uwezo wa kupata ardhi unapaswa kuwa haki ya wafanya kazi itakayowaruhusu kujipatia maskani na chakula.

Tunapoangalia uandikishaji wa wanachama wa vyama vya wafanya kazi katika baadhi ya nchi (kwa mfano Kenya, ambako ule mradi wa mkulima ndogo ulifanyia utafiti), inatubidi kutambua kwamba vyama vya wafanya kazi huenda visiwe na wakati au fedha au njia zifaazo za mawasiliano kufanya kampeni za uandikishaji katika kiwango cha kitaifa. Ikiwa wakulima wadogo na wafanya kazi wao hawajapangwa, wanapaswa kupewa nyenzo kuwawezesha kufanya hivyo. Uwezeshaji wa kupitia kitendo cha pamoja unaweza kuanza utaratibu huo, ukiwa na wahamasishaji watendaji wasio na utaalamu wanaoishi katika jamii za vijijini (kwa mfano wafanya kazi wa viwanda vya kutengeneza bidhaa) kama washiriki muhimu. Wanapaswa kuhimizwa kufanya kampeni ya kuwaandikisha wakulima wadogo na wafanya kazi wao katika vyama vya wafanya kazi. Hii pia itakuwa njia rahisi ya kukusanya ada kutoka kwa wakulima wadogo na wafanya kazi.

International Co-operative Alliance, ni shirika la kimataifa lisilo la kiserikali linalo- unganisha na kuwakilisha vyama vya ushirika kote ulimwenguni. Shirika hili linaweza kutoa jawabu kwa baadhi ya wakulima wadogo, wawe waajiri au wengineo. Shirika hili lina uwezo mkubwa wa kimataifa likiwa na zaidi ya mashirika wanachama 230 yakiwakilisha watu milioni 760 kote ulimwenguni. Lengo lake kuu ni kusaidia na kuvipa nguvu vyama vya ushirika vilivyofaulu vinavyorahisisha maendeleo ya mahusiano ya kiuchumi na mengineyo baina ya mashirika wanachama. Pia shirika hili huasisi vyama vipya vya ushirika. Linaweza kuwapa wanachama na wenzao, mtandao wa mawasiliano ili waweze kupata maarifa na changamoto ya utendaji bora kutoka kwa wengine.

7.5 Tafiti mbalimbali

Vyama vya wafanya kazi ulimwenguni kote vimewapanga wakukulima wadogo kwa njia ya kudumu. Baadhi ya mifano imeorodheshwa kama ifuatavyo.

UNAC, Colombia

Chama cha Colombia UNAC (National Agro-Food Union) kinawakilisha sekta mbalimbali katika mtungo wa chakula na kilimo, vyama vya wazalishaji wadogo na mashirika yanayohusika na mafunzo ya uhifadhi wa mazingara, pamoja na uzalishaji wa kilimo na ikolojia. Kiliasisiwa mnamo mwaka wa 2000 kwa usaidizi wa IUF. Katika kipindi cha miaka miwili, kilikuwa kimeasisi mashirika 756 na wanachama 74000. Dhima yake sio tu kujadili na kutetea maafikiano ya pamoja bali kuingilia katika kiwango cha kitaifa pamoja na serikali kutimiza mahitaji ya watu wa vijijini. Huwa kinaandaa mafunzo yanayohusisha familia nzima ambapo jamaa wanajadiliana mambo ya ikolojia, uzalishaji wa kilimo wa kudumu, usimamizi na udhibiti wa kijamii wa ardhi isiyotumika kwa kilimo (yaani ulinzi wa misitu, maji na vichaka) na mafunzo ya masuala ya mazingira. Pia huwa wanawapanga wafanya kazi huru na familia zao kuzalisha na kuuza nje ndizi kama wanachama wa vyama vya ushirika. UNAC inatafuta usaidizi kutoka kwa serikali na jamii ya kimataifa ili kuimarisha mpangilio na kazi ya mitandao hii.

CONTAG, Brazil

Huko Brazil CONTAG (National Confederation of Agricultural Workers) ina vyama vya wafanya kazi 2700 na wanachama milioni 10 ambao kwa miaka 40 wamefanya kampeni ya mabadiliko ya umiliki wa ardhi, sera za ufadhili, uuzaji, haki za ajira ikiwa ni pamoja na sera za ujana, sera mbalimbali za kilimo kwa wakulima wenye familia, na marupurupu ya kijamii (ikiwa ni pamoja na pensheni/malipo ya uzeeni) kwa wafanya kazi wa vijijini. Ili kuhakikisha kuwa vyama vya wafanya kazi vinahusika katika utaratibu huu, CONTAG imeona ni lazima ihusishe jamii kwenye utaratibu wa kufanya maamuzi yasio ya mikoani. Hivyo imechagua Viranja (madiwani) na wanachama 10014 wa mabaraza ya vijijini.

Uruguay

Huko Uruguay kaskazini, mpakani wa pamoja na Brazil, wakulima wadogo huzalisha mboga katika nyumba za vioo. Miaka mitano iliyopita wakazi walikuwa na madeni mengi na walitegemea teknolojia ya pembejeo zilizokuwa ghali na zenye kuchafua mazingira. Kwa kila masanduku 10 ya nyanya, manne yalitumiwa kulipia viuadudu. Kwa usaidizi wa IUF ya mkoani, wakulima wamebadilisha hali hii kwa kujenga muungano ambapo wanafanya kazi pamoja katika mazingira wanatotuzwa viumbe na mazingira.

PKSK, Philippines

PKSK (National Union of Independent Rural Organisations) ni shirika jipya lililoanzishwa kutokana na utandawazi na kutorekebishwa kwa uchumi. Miungano ilijengwa na Akbayan (chama cha upinzani kilichoshinda kiti katika uchaguzi uliopita kwa kutetea sera za mabadiliko ya umiliki wa ardhi na maendeleo ya vijijini), PAKISAMA (shirikisho la kitaifa la wafanya kazi wa shamba) na KASAMALO (shirikisho la kitaifa la wafanya kazi wa shamba wa kidemokrasia).Kupitia miungano hii PKSK inawakilisha wakulima wadogo, wafanya kazi shambani, wavuvi, wanawake, wenyeji na vyama vya ushirika. PKSK imeanzishwa katika mikoa 20 kati ya 76 huko Ufilipi. Lengo lake ni kuboresha njia ya uzalishaji, huduma na masoko, kuinua hali ya mawasiliano baina ya viongozi na kuwapa mafunzo zaidi.

7.6 Ajira ya watoto

"Bitter harvest", ni hati ya ILO kuhusu ajira ya watoto katika kilimo iliyotolewa mnamo mwaka wa 2002. Hati hii inasema kwamba, "kazi inayofanywa na watoto katika kilimo mara nyingi haionekani, kwa sababu watoto huwa wanawasaidia wazazi wao katika kazi. Huwa haijulikani kwa kuwa kazi yao haitambuliwi au kurekodiwa kwa urahisi katika takwimu, Hii inasababisha mzunguko wa umaskini na huathiri maisha ya baadaye ya watoto kwa kuwa uwezo wao wa kupata elimu na mafunzo umepunguzwa mno". Nusu ya maafa yanayotokea kazini huwa katika kilimo na mengi yahusu watoto kulingana na takwimu. Idadi kubwa zaidi ya watoto wenye umri wa kati ya miaka 5 na 4 (yapata asilimia 40) wanaofanya kazi wamo barani Afrika, ambako imo idadi kubwa zaidi ya watoto katika sehemu za mashambani/vijijini, hususan wasichana. Kwa mfano, inaaminika kwamba watoto hujumuisha robo ya wafanya kazi wote wa kilimo nchini Kenya. Ripoti ya hivi punde ya ILO inasema kuwa karibu theluthi moja ya wafanya kazi wa kilimo ni watoto katika baadhi ya mataifa yanayoendelea. Kuongezeka kwa idadi ya mayatima waliopoteza wazazi wao kutokana na ukimwi kutasababisha ongezeko kubwa la idadi hii iwapo hatua hazitachukuliwa kukomesha ukimwi.

Vyama vya wafanya kazi vimeshughulikia suala hili kwa uzito kabisa. CONTAG (Brazil) na GAWU (General Agricultural Workers Union, Ghana) wamekuwa katika mstari wa mbele wa vita dhidi ya ajira ya watoto kama inavyoonyeshwa na mifano ifuatayo:

CONTAG, Brazil

- Walitoa nakala 10,000 za *Child workers programme* mnamo mwaka wa 1993 ili kusambaza habari kuhusu haki za watoto wa vijijini na kuwafunza wanachama wa vyama vya wafanya kazi jinsi ya kuboresha nafasi za maafikiano ya pamoja (CBAs) kuhusu kukatazwa kwa ajira ya watoto.
- Walitoa kozi 5 za mafunzo kwa viongozi 150 wa vyama vya wafanya kazi, pamoja na vipindi 7 vya redio ili kuleta utambuzi. Vipindi hivyo vilipeperushwa hewani kwenye tovuti yaCONTAG yenye vituo? 160 vya redio.
- Waliwaleta wazazi na watoto wanaofanya kazi pamoja ili kujadili hali za kimaisha na kikazi za watoto wa vijijini. Haya yote yalisaidia kushawishi serikali kuidhinisha ILO C182, jambo ambalo lilifanyika hapo mwaka wa 2000.
- Walianzisha tume kuonyesha aina mbaya zaidi za ajira ya watoto. Sasa wanaipa serikali changamoto ya kuunda sera za umma ili kutekeleza ILO C138 na C182. Hatua walizopendekeza ni: kuleta utambuzi miongoni mwa wabunge, majaji, waajiri, wazazi na watoto; mabadiliko ya umiliki wa ardhi; ulinzi wa kijamii wa kimataifa; mipango ya misaada ya masomo ambapo familia maskini ambazo hazifanyi kazi zinalipwa mshahara wa chini kabisa iwapo watawapeleka watoto wao shuleni.

GAWU, Ghana.

- Walijadili CBA na kamati ya Ghana Oil Palm Development, ili kuitumia kukomesha ajira ya watoto kwenye mashamba makubwa na nchini kwa jumla.
- Walifanya utafiti wa pamoja kuhusu ajira ya watoto.
- Walitoa mafunzo na elimu; walianzisha mipango ya tuzo na vikwazo hasa kwa vibarua, wakulima wadogo na wakulima wa kandokando.
- Walizidisha utambuzi kuhusu ajira ya watoto na uhusiano wake na haki za wanawake, watoto, wafanya kazi na binadamu pamoja na maendeleo ya kudumu.

Vyama vya wafanya kazi lazima vitumie hoja kwamba kilimo kinachotegemea ajira ya watoto si cha kudumu. Ron Oswald, ambaye ni katibu mkuu wa IUF, anasema kwamba, "watoto hufanya kazi kwa sababu wazazi wao ni maskini; ni lazima wajalize mapato ya familia au wafanye kazi bila malipo. Ajira ya watoto katika kilimo haiwezi kushughulikiwa peke yake bila ya kushughulikia mojawapo ya vyanzo vyake vikuu, yaani, umaskini vijijini. Vyama vya wafanya kazi vinaweza kufanya kazi kuondoa ajira ya watoto lakini kipaumbele kikuu lazima kiwe ni

kuinua hali za kimaisha na kikazi za wafanya kazi nyumbani. Kwa kufanya hivi, vitaondoa haja ya watoto kufanya kazi. Ajira ya watoto ya bei rahisi inadhoofisha uwezekano wa kujadiliana ujira wa haki unaofaa kwa wafanya kazi waliokomaa.. Ni sharti tufanye kazi kuondoa ajira ya watoto ili kuuvunja mzunguko wa umaskini vijijini".